

Haki na Ulinzi Wako Dhidi ya Bili Zisizotarajiwa za Matibabu

Unapopata matibabu ya dharura au kutibiwa na mtoa huduma wa nje ya mtandao katika hospitali au kituo cha upasuaji usiohusisha kulazwa hospitalini cha mtandao, unalindwa dhidi ya kutozwa bili isiyotarajiwa au bili ya salio.

Je, “kutozwa bili ya salio” (wakati mwingine huitwa “kutozwa bili isiyotarajiwa”) ni nini?

Unapohudumiwa na daktari au mtoa huduma mwingine wa afya, unaweza kudaiwa baadhi ya gharama za kulipia mwenyewe, kama vile malipo ya mshiriki, malipo ya kushirikiana na bima, na/au makato. Unaweza kuwa na gharama zingine au kulazimika kulipa bili yote ikiwa utahudumiwa na mtoa huduma au kutembelea kituo cha afya ambacho hakipo katika mtandao wa mpango wako wa afya.

“Wa nje ya mtandao” inamaanisha watoa huduma au vituo ambavyo havijafanya mkataba na mpango wako wa afya. Watoa huduma wa nje ya mtandao wanaweza kuruhusiwa kukutoza bili ya salio linalobaki kati ya kiasi ambacho mpango wako wa afya ulikubali kulipa na kiasi kamili kinachotozwa kwa huduma. Hili linaitwa “**kutozwa bili ya salio.**” Kiasi hiki kina uwezekano wa kuwa zaidi ya gharama za mtandaoni kwa huduma sawa na kinaweza kutojumuishwa katika kikomo chako cha gharama za kulipa mwenyewe cha kila mwaka.

“Kutozwa bili isiyotarajiwa” ni bili ya salio isiyotazamiwa. Hili linaweza kufanyika wakati huwezi kudhibiti anayehusika katika matibabu yako—kama unapokuwa na dharura au unapopanga ziara katika kituo cha mtandao lakini kutibiwa na mtoa huduma wa nje ya mtandao bila kutazamia.

Unalidwa dhidi ya kutozwa bili ya salio kwa:

Huduma za dharura

Ikiwa una maradhi ya dharura na upate huduma za dharura kutoka kwa mtoa huduma au kituo cha nje ya mtandao, kiasi cha juu zaidi ambacho mtoa huduma au kituo hicho kinaweza kukutoza bili ni kiasi cha gharama za kushirikiana za ndani ya mtandao cha mpango wako (kama malipo ya mshiriki na malipo ya kushirikiana na bima). **Huwezi** kutozwa bili ya salio kwa huduma hizi za dharura. Hizi ni pamoja na huduma unazoweza kupata baada ya hali yako kuimarika, isipokuwa ukitoa idhini iliyoandikwa na kuacha ulinzi wako wa kutotozwa bili ya salio kwa huduma hizi za baada ya kuimarika.

Baadhi ya huduma katika hospitali au kituo cha upasuaji usiohusisha kulazwa hospitalini cha mtandao

Unapopata huduma kutoka kwa hospitali au kituo cha upasuaji usiohusisha kulazwa hospitalini cha mtandao, watoa huduma fulani wanaweza kuwa wa nje ya mtandao. Katika hali hizi, kiasi cha juu zaidi ambacho watoa huduma hao wanaweza kukutoza bili ni kiasi cha gharama za kushirikiana za ndani ya mtandao cha mpango wako. Hili hutumika katika dawa, nusukaputi, patholojia, rediolojia, maabara, huduma za watoto wachanga, mpasuaji msaidizi, mhudumu

wa hospitali, au huduma za tabibu wa uangalizi makini za dharura. Watoa huduma hawa **hawawezi** kukutoza bili ya salio na **hawafai kamwe** kukuomba uache ulinzi wako wa kutotozwa bili ya salio.

Ikiwa utapata huduma zingine katika vituo hivi vya mtandao, watoa huduma wa nje ya mtandao **hawawezi** kukutoza bili ya salio isipokuwa ukitoa idhini yako iliyoandikwa na kuacha ulinzi wako.

Huhitajiki kamwe kuacha ulinzi wako dhidi ya kutozwa bili ya salio. Pia huhitajiki kupata huduma nje ya mtandao. Unaweza kuchagua mtoa huduma au kituo kilicho katika mtandao wa mpango wako.

Wakati ambapo kutozwa bili ya salio hakuruhusiwi, pia una ulinzi unaofuata:

- Unawajibika tu kulipa sehemu yako ya gharama (kama malipo ya mshiriki, malipo ya kushirikiana na bima na makato ambayo ungelipa ikiwa mtoa huduma au kituo kingekuwa cha mtandao). Mpango wako wa afya utalipa watoa huduma na vituo vya nje ya mtandao moja kwa moja.
- Mpango wako wa afya kwa kawaida lazima:
 - Ulipie huduma za dharura bila kukuhitaji kupata idhini ya huduma kwanza (idhini ya awali).
 - Ulipie huduma za dharura kutoka kwa watoa huduma wa nje ya mtandao.
 - Uweke kiasi unachodaiwa na mtoa huduma au kituo (kugawana gharama) kulingana na kiasi ambacho ungemlipa mtoa huduma au kituo cha mtandao na kuonyesha kiasi hicho katika ufafanuzi wako wa mafao.
 - Ujumuishe kiasi chochote unacholipa kwa huduma za dharura au huduma za nje ya mtandao katika kikomo chako cha makato na malipo ya kulipia mwenyewe.

Ikiwa unaamini umetozwa bili kimakosa, au unataka maelezo zaidi, unaweza kupiga simu kwa 1-800-985-3059.

Tembelea <https://www.cms.gov/nosurprises> kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako chini ya sheria ya shirikisho.